

# Salim aendelea

Uchurukuzi, 7th January, 13-9-84, Page 7.

# kuhimiza kilimo

Waziri Mkuu, Ndugu Salim Ahmed Salim amewataka Watanzania wote wanaoishi kwenye mikoa ilio na ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha kutumia uwezo wao wote kuzalisha mazao ya chakula na biashara kwa wingi, ili kuondoa uhaba wa chakula nchini na kuliungezea taifa uwezo wa kupata fedha za kigeni.

Alisema kuwa njia ya kuondoa umaskini ambao unalikabili taifa na wananchi wake ni kuzidisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Waziri Mkuu alikuwa akihutubia mukano wa hadharaj miini Liwale jana akiba katika ziara ya siku tano

mkoani Lindi ambayo inamalizika leo.

Alisema katika ziara yake mkoani Lindi ameona maeneo makubwa ya ardhi yenye rutuba ambayo, kama yangetumika kikamilifu, mikoa huo ungekuwa mionganoni mwa mikoa inayozalisha mazao mengi ya chakula na biashara.

Akifafanu kuhusu suala la fedha za kigeni, ambalo limekuwa likiwatatanisha watu wengi, alisema, fedha za kigeni sio kiu cha ajabu ambacho kipo hewani, bali maana yake ni uwezo wa taifa kuza mazao yake nchini za nje.

Waziri Mkuu alisema mazao

yanayouzwa nje ndiyo yanayoliwesha taifa kubadilishana na bidhaa muhimu kutoka nje zinazohitajika kwa ajili ya mpango ya maendeleo na miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa barabara ya Kibiti-Lindi ambayo inahitaji kiasi kikubwa cha fedha za kigeni.

Mapema Waziri Mkuu alitembelea duka la ushirika linalomilikiwa na chama cha walaji cha mijini Liwale na pia alikagua miradi wa ng'ombe wa kijiji cha Makata ambacho kwa upande wa ufugaji kimefikia hatua ya mwanzo kuwa na ng'ombe 84.

Kuhusu ujenzi wa shule za sekondari, zinazojengwa kila wilaya chini ya mpango wa taifa, kwa

kupanua elimu ya sekondari, Waziri Mkuu aliwapongeza Watanzania kwa kutambua umuhimu wa shule hizo na kuweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wake kwa njia ya kujitolea.

Vijiji na mashirika ya umma wilayani Liwale vilimkabidi Waziri Mkuu mchango wa jumla ya sh. 62,403 kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo ambayo tayari wananchi wamefyatua jumla ya matofali 550,000 katika kipindi cha majumaa sita.

Leo Waziri Mkuu atakwenda Nachingwea ambako atazungumza na viongozi wa Chama na Serikali wa mikoa wa Lindi kabla ya kurejea Dar es Salaam.